



## Tarifa kwa umma

### Utafiti mpya unaonyesha ufinyu wa taarifa na ushiriki hafifu katika elimu miongoni mwa wazazi

Kiwango cha taarifa walichonacho wazazi kuhusu sera muhimu za elimu na utekelezaji wake ni cha chini mno, hali inayoashiria uwezekano mkubwa wa wazazi kushindwa kudai au kushiriki katika kuchangia ubora wa ufundishaji na ujifunzaji wa watoto wao. Matokeo haya yamo katika muhtasari wa sera uitwao “Dar es Salaam wanaichukuliaje elimu? Uelewa, maoni na ushiriki wa wazazi Dar es Salaam”.

Muhtasari huo unatokana na utafiti uliofanywa mwaka 2010 na Uwazi—Twaweza ikishirikiana na DataVision miongoni mwa kaya 429 zilizochaguliwa kinasibu mkoani Dar es Salaam. Utafiti huo umebaini kuwa asilimia 97 ya wazazi hawajui kuhusu ruzuku kwa kila mwanafunzi (*capitation grant*); na pia kwamba hawajui kiwango cha ruzuku hiyo ambacho serikali inapaswa kupeleka shuleni katika mwaka wa masomo. Walipoulizwa kuhusu matokeo ya mitihani ya karibuni ya kumaliza elimu ya msingi katika shule wanazosoma watoto wao, zaidi ya asilimia 80 hawakuwa na taarifa yoyote. Aidha, zaidi ya asilimia 50 ya wazazi hawakuwahi kuhudhuria mkutano hata mmoja wa kamati ya shule katika kipindi cha mwaka mmoja kabla ya utafiti.

Idadi hii kubwa ya wazazi wasiofahamu kuhusu masuala muhimu yanayoathiri matokeo ya kujifunza katika shule za watoto wao ni ishara ya udhaifu katika mfumo mzima wa kupashana taarifa na uwajibikaji katika elimu. Watu wasio na taaarifa za kutosha kuhusu nyenzo muhimu mashuleni hawawezi kudai au kuchangia kwa ufanisi katika kuboresha ufundishaji au mazingira ya kujifunzia shuleni kwa watoto wao.

Ufinyu wa taarifu miongoni mwa wazazi unahatarisha utekelezaji wa sera za kuboresha elimu. Nyankomo Marwa, Afisa Mtafiti wa Twaweza anaeleza zaidi:

“Kwa kawaida watoa huduma wanapotoa huduma mbovu watumiaji huamua kuacha kuzitumia na kutafuta huduma mbadala. Lakini kwa sababu wazazi hawana taarifa kamili kuhusu hali ya elimu katika shule wanazosoma watoto wao, inakuwa vigumu kwao kuwahamishia shule nyingine zinazoweza kuwa zinafundisha vizuri zaidi.

Pamoja na changamoto zilizotajwa hapo juu, utafiti umebaini kuwa asilimia 44 ya wazazi wanaridhishwa na elimu inayotolewa na karibu asilimia 60 wanaridhishwa na hali ya miundombinu ya shule hasa majengo. Aidha, idadi kubwa ya wazazi walisema, wangepata taarifa husika, wako tayari kuchukua jukumu zaidi katika kufuatilia ubora wa elimu na matokeo ya ujifunzaji.

Matokeo haya ni changamoto kwa wananchi, ambao kupitia ushiriki makini, wanaweza kuleta ufumbuzi wa tatizo la upashanaji wa taarifa na kulegalega kwa uwajibikaji katika sekta ya elimu. Jitihada kama hizi pia zitasaidia kupanua uelewa, uwazi na kufanya wananchi zaidi wachukue hatua katika kufuatilia na kudumisha ubora wa ujifunzaji na matokeo ya elimu.

Wahusika wengine pia wana michango ya kutoa. Kwa mfano, serikali inapaswa kuhakikisha kuwa taarifa juu ya migawo ya ruzuku na sera mbali mbali za elimu zinasambazwa kwa upana zaidi. Wahisani, vyombo vya habari na mashirika ya kiraia wanapaswa kufanya kazi kwa pamoja na serikali katika kusambaza taarifa husika. Pia wanataaluma na mashirika ya kiraia wanapaswa kuwekeza zaidi katika tafiti zinazotoa ushahidi wa msingi, ili kutambua ni sehemu gani za mfumo hazifanyi kazi na kusambaza matokeo ya tafiti hizo kwa wadau muhimu.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Nyankomo Marwa, Afisa Mtafiti, Uwazi—Twaweza kupitia: [nmarwa@twaweza.org](mailto:nmarwa@twaweza.org). Muhtasari huu unaweza kupakuliwa kutoka [www.twaweza.org/go/Uwazi](http://www.twaweza.org/go/Uwazi).

**Mwisho**